

**TAARIFA YA MRADI WA KITUO KIDOGO CHA KUPOZEA UMEME SAHARE
KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA,**

NDUGU JUMA ALI SIMAI

TAREHE 16 MEI 2013.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi wa kituo cha kupozea umeme cha hapa Sahare, ni mmoja wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Mfuko wa Changamoto za Millenia (MCC) na kusimamiwa kwa niaba ya serikali na Mfuko wa Changamoto za Milenia Tanzania (MCA-T). Ujenzi wa kituo hiki umefanywa na kampuni ya Symbion ya Marekani kwa kushirikiana na kampuni ya Alstom Grid ya Ufaransa. Mhandisi mshauri ni kampuni ya ESBI kutoka Ireland.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha Sahare ulianza rasmi Januari 2011 na unategemewa kumalizika katikati ya mwezi Juni 2013. Kituo hiki cha kupozea umeme wa msongo wa kati (33/11kV) kina ukubwa wa 15MVA. Jumla ya wateja wa mwanzo zaidi ya mia mbili wanategemewa kuaunganishwa mara tu ujenzi wa kituo hiki utakapokamilika. Vivyo hivyo wateja wapatao elfu tano katika eneo hili, zikiwemo hoteli kubwa tatu, hospitali moja, zahanati mbili, chuo cha ualimu kimoja, shule za sekondari tisa na shule za msingi tatu, wataweza kupata umeme wa uhakika baada ya ujenzi wa kituo hiki kumalizika.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu hadi kukamilika kwake utagharimu dola za Kimarekani (USD) **1,541,408.95**. ambazo ni takribani shilingi billion 2.5 za Tanzania.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Miradi mingine ambayo inafadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia MCC katika mkoa wa Tanga na iko katika hatua za mwisho za ukamilikaji ni kama ifuatavyo:

- Mradi wa Ujenzi wa Ukarabati na Upanuzi wa Miundombinu ya kusambazia Umeme katika mkoa wa Tanga wenye jumla ya kilometa 53 za msongo wa kati (medium voltage) na msongo mdogo (Low Voltage) kilometa 176 na upo katika wilaya za Handeni,

Korogwe, Muheza, Lushoto, , Pangani na Tanga na unajumuisha vijiji 80 na mitaa kadhaa.

- Mradi wa ujenzi wa vituo vya kupozea umeme ambavyo ni Kasiga katika wilaya ya Korogwe, Kange kilichopo karibu na kiwanda cha saruji cha Tanga (Simba cement), Songa wilayani Muheza na hiki cha Sahare,

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Miradi hii inatekelezwa kwa madhumuni ya kuimarisha na kupanua miundombinu ya usambazaji wa umeme katika juhudi za kufikisha umeme wa uhakika kwa watumiaji wa zamani na wapya. Faida nyingine katika miradi hii ni pamoja na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Nimalizie kwa kuwaomba Viongozi wa Serikali katika Mkoa wa Tanga na wananchi wa Tanga, kutoa ushirikiano kwa TANESCO katika kuhakikisha miundombinu ya umeme pamoja na hii mipya inalindwa. Uzoefu katika miradi mingine mipya unaonesha kuwa kumekuwa na wananchi wachache wenye tabia za udokozi wa nyaya na mafuta ya transfoma. Vitendo hivi vinachangia uharibifu mkubwa wa miundombinu iliyowekwa kwa gharama kubwa sana na kuzorotesha juhudi za Serikali za kuwapatia wananchi huduma hii muhimu ya umeme.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Tunaomba sasa utuwekee jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huu wa *kituo cha kupozea umeme cha Sahare*.

ASANTENI